ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (263-273), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Tija za Mwangwi wa Falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika Riwaya ya Kufikirika

Rehema Hassan Koshuma[1*], Dkt. Hadija Kutwa Abdallah[2]

[1*]Barua pepe; Simu

[2]Barua pepe; Simu

DOI: https://doi.org/10.5281/zenodo.23614491

Published Date: 24-October-2026

IKISIRI: Utafiti huu unahusu kuchambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika riwaya ya *Kufikirika*.Utafiti huu uliongozwa na lengo mahususi moja ambalo ni: Kuchambua Tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika riwaya ya Kufikirika. Kwa kuzingatia lengo la utafiti huu, mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data ni mbinu ya udodosaji na mbinu ya usomaji maktabani. Kwa kutumia mbinu hizi mbili, data zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli yaani, maelezo yalizingatiwa katika uchambuzi wa data. Uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Elimu Jamii iliyoasisiwa na Hippolyte Taine (1864).Utafiti wa makala haya ulitumia sampuli ya riwaya moja ya Kufikirika na watafitiwa kumi. Utafiti wa makala haya ulitumia Usampulishaji lengwa tajwa mpokezano. Kupitia mkabala wa kitaamuli, uwasilishaji wa matokeo ya utafiti yameonesha kuwa, tija zamwangwi wa falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika riwaya ya Kufikirika ni kama ifuatavyo: Husaidia kuponesha maradhi mbalimbali kupitia matumizi ya dawa za asili, husaidia katika ulinzi wa jadi kupitia mazindiko na dawa za asili. Pia, husaidia kudumisha mila na desuri za jamii kupitia utekelezaji wa matambiko na uganga, husaidia kuleta mvua kupitia utekelezaji wa matambiko ya mvua. Vile vile, husaidia jamii kuishi kwa amani na utulivu kupitia masuala ya ugangana matambiko, husaidia kustawisha mazao kupitia utekelezaji wa kafara na matambiko. Husaidia jamii kuishi kwa kuaminiana kupitia viapo na masuala ya uganga, husaidia kudumisha umoja na mshikamano katika jamii kupitia shughuli mbali mbali za kijamii. Pia, husaidia kuleta utawi wa familia kupitia masuala ya ndoa na uzazi, husaidia kuongeza ukoo kupitia falsafa ya familia pana.

1. UTANGULIZI

Maisha ya kila jamii yamejengwa na falsafa yake. Hii ni kutokana na kuwa, pamoja na kuwa na ufanano kati yajamii moja na nyingine, pia kuna mambo mbalimbali yanayotofautisha jamii moja na nyingine. Ikiaminiwa kuwa falsafa ni upendo au hekima, kufikiri kwa kina zaidi kimpangilio kuhusu asili ya ujumla ya ulimwengu au ukweli, hoja juu ya imani, kuwepo kwa maisha na hoja sahihi kama wasemavyo Nyiremba na Ishumi (2004). Imeonekana kuwa, falsafa ilianza pindi binadamu alipoanza kustaajabu ulimwengu na kuhitaji majibu ya maswali juu ya maana kama vile kuumbwa kwa bindamu.

Ni dhahiri kuwa, falsafa ni jambo linalohusiana na uwezo wa akili katika kufikiri kwa kina na mantiki katika kufanya utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazomkabili mwanadamu katika maisha yake ya kila siku na hii ndio falsafa yenyewe. Mawazo haya yameungwa mkono na Johnston (2006), akieleza kuwa, falsafa lilikuwa ni jambo la kushughulikia matatizo ya kiitikeli (desturi za jamii). Hivyo, inaleta ushawishi kuwa, ili kufanya uchunguzi sahihi wa kiitikeli, ni sharti muhusika awe na maarifa sahihi, kwa hiyo, falsafa ilihusika na kujiuliza maswali kama vile ninajuaje? Na ninajua nini? Kwa maana hiyo basi, ili uwe na falsafa, ni lazima kwanza uwe na maarifa na maadili sahihi katika kushughulikia matatizo. Kwa mantiki hii, kutokana na kuwepo kwa mapito ya hatua mbalimbali za maisha kati ya jamii moja na jamii nyingine, kumesababisha kuwepo kwa falsafa tofauti tofauti katika jamii hizo.

Kwa mfano, falsafa ya Uplato ina nafasi kubwa katika jamii ya kimagharibi.Inaaminika kusema, Plato ni mwanafalsafa mwenye ushawishi kupitia mitazamo yake kuhusu uhalisia wa kuwepo kwa Mungu katika maisha ya mwanadamu (Nails,

2002). Plato alifasili maisha kuwa, ni umbo linalojengwa na mambo mema, hali na yaliyo umuhimu kwa mwanadamu, ambayo humfanya kuwa na fikra za kifalsafa kwa kuwa na elimu ya kweli (Cooper, 1997).

Mnamo karne ya 20, iliibuka falsafa ya maisha ya Kipragmatiki iliyosisitiza kukubali mazingira, ili kuishi maisha ya ukweli (Menand, 1998). William James ni muumini wa falsafa hii anayeeleza kuwa, falsafa ya maisha iliyo bora ni ile inayofasiri maisha kupitia vitu halisi kuliko mtazamo wa kiakili. Kwa mantiki hiyo, falsafa ya maisha ya Kipragmatiki kwa mujibu wa Menand (1998), imejiegemeza katika uyakinifu siyo udhanifu, yaani vitu vya kushikika. Kwa kuwa fasihi ni kapu la kuhifadhi amali zote za jamii, Shaaban Robert ni mwandishi mahiri wa kazi za fasihi ya Kiswahili aliyejitokeza kueleza falsafa ya maisha ya Afrika na Afrika ya Mashariki kwa uzoefu wake.

Kwa mfano, Chuachua (2016), alizungumzia falsafa ya maisha ya Waafrika kwa mwegamo wa Epistemolojia ya Kibantu kupitia riwaya za Shaaban Robert. Bila shaka falsafa ya maisha ya kila jamii, hudhihirika katika amali za jamii husika. Kwa mnasaba huu, kazi za fasihi kama riwaya, tamthiliya na ushairi, zimekuwa chombo muhimu cha kufafanua falsafa ya maisha ya jamii kama Wapare. Mwandishi wa kazi za fasihi huathiri au kuathiriwa na jamii yake. Yaani mazingira yaliomkuza na kumlea, ndiyo yanayomchagulia aina ya fasihi ya kuandika. Kwa kuwa Shaaban Robert ni mtu aliyekuzwa na ukanda wa Pwani ya Afrika ya Mashariki, hasa Tanga.

Ukiachilia maelezo ya Chuachua (2016), kusema riwaya za Shaaban Robert zilielezea falsafa ya Kiafrika kwa ujumla wake, lakini ilitazamiwa kazi zake zielezee zaidi falsafa ya watu wa Pwani kwa kuwa yeye ni mtu wa Pwani. Wakati zikiangaliwa kwa jicho pevu, riwaya hizo zinaonekana kuwa na mwangwi wa kifalsafa baina yake na jamii ya Wapare kwa umahususi. Yaani, riwaya za Shaaban Robert zinaendana sambamba na falsafa ya jamii ya Wapare. Makala haya yamelenga kubaini mwangwi wa falsafa ya Wapare unaodhihirika katika riwaya ya Kufikirika kwa kuzingatia lengo moja. Lengo hilo ni kubaini miktadha inayodhihirisha falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika.

Wapare ni kabila linalopatikana miongoni mwa mikoa ya kaskazini mwa nchi ya Tanzania, mahususi mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Same vijijini katika kijiji cha Vuje, kitongoji cha Mgambo. Wapare wapo katika wilaya ya Moshi sehemu za Himo na Chekereni. Kutokana na shughuli za kiuchumi, Wapare wamesambaa katika maeneo mbalimbali na hivyo, kusababisha mwingiliano na kabila la Wasambaa waliopo katika milima ya Usambara na maeneo ya baadhi ya vijiji vilivyopo katika mkoa wa Tanga kama vile Lushoto na Handeni.

Wapare wanajishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile kilimo, ufugaji, biashara na ujira, masuala ya kisiasa na shughuli mbalimbali za kiutamaduni kama zilivyo jamii nyingine za Kiafrika.

Makala haya yametumia riwaya ya Kufikirika iliyoandikwa na Shaaban Robert (1967), ili kuonesha namna iliyokuwa na mwangwi wa falsafa ya jamii ya Wapare, kwani, yaliyoelezwa ndani ya riwaya hii yana uhusiano wa moja kwa moja na mambo yanayotendeka katika jamii ya Wapare, pamoja na kuwa Shaaban Robert ni mtu wa Pwani. Yaani, maudhui ya Kufikirika yana uhusiano na jamii za maeneo mengine nje ya Pwani ikiwemo jamii ya Wapare wa pande za Kaskazini mkoani Kilimanjaro, wilaya ya Same vijijini, mahususani kijiji cha Vuje katika Kitongoji cha Mgambo.

Ikiwa riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari na yanayoeleza ukweli fulani katika maisha kama wasemavyo TUKI (2002). Ni dhahiri kuwa, riwaya ni masimulizi yanayoeleza ukweli wa mambo fulani ya maisha ya mwanadamu. Hata maelezo haya yamepata kuungwa mkono na Madumula (2009), kuwa, riwayani ile ambayo inafungamana na utamaduni wa jamii ambayo hupatikana katika nchi ya Afrika Mashariki. Ni ile yenye lugha ya kinathari, inasawiri maisha ya jamii, masimulizi ya kubuni na visa virefu, wahusika zaidi ya mmoja na mpangilio wa msuko wa matukio.Maelezo haya yameshadadiwa na Senkoro (1982), akieleza kuwa, riwaya ni mchanganyiko au mkusanyiko wa visa vyenye urefu unaoviruhusu vitambe na kutambaa mahali pengine apendavyo mwandishi wake. Hoja hii ni dhahiri kuwa, mtunzi wa kazi za kifasihi anapoandika kazi zake, huguswa na mambo mbalimbali yaliyopo ndani ya jamii husika. Mambo hayo huweza kuangaliwa katika mtazamochanya na/au hasi kwa jamii. Makala haya yamechambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika ili kuweka wazi tija za falsafa ya jamii ya Wapare.

2. KIUNZI CHA NADHARIA

Wataalamu mbalimbali wameelezea kuhusu kiunzi cha nadharia katika kazi za fasihi kama ifuatavyo:

Kiunzi cha nadharia ni mawazo ambayo humuongoza mtu katika kutenda (TUKI, 2014). Hata maelezo haya yametiliwa mkazo na Ponera (2016), akieleza kuwa, kiunzi cha nadharia ni namna ya utumiaji wa nadharia katika kazi za kitafiti. Mtafiti hutumia misingi yanadharia teule katika kuunda malengo.Kiunzi cha nadharia humsaidia mtafiti katika kulinda

duara la utafiti. Nadharia ya Elimu Jamii iliyoasisiwa na Hippolyte Taine (1864), katika kitabu chake kilichoitwa *History of English Literature* ilitumika katika makala haya. Kutokana na anguko la kiuchumi huko Ulaya katika karne ya 19, kulisababisha kuasisiwa kwa nadharia ya Elimu Jamii. Nadharia ya Elimu Jamii imeeleza kuwa, elimu jamii ni jumla ya masuala yote yanayoihusu jamii kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi. Nadharia hii imeweka msisitizo zaidi katika kueleza masuala ya kijamii. Makala haya yameelezea masuala ya kijamii kupitia mchakato wa kuchambua mambo mbalimbali yanayotendeka katika jamii.

Lengo kuu la nadharia hii ni kuchambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare zinazodhihiririka katika riwaya ya Kufikirika. Nadharia ya Elimu Jamii imejengwa kwa misingi sita ambayo ni: msingi wa dhana / fikra, msingi wa daraja la mabadiliko katika mifumo, msingi wa hisia, kukubalika kwa sharia maalumu na sababu zake, msingi wa fasihi kama chombo cha ukombozina msingi wa sanaa na jamii/fasihi na jamii.Misingi mmoja wa nadharia ya elimu jamii ulitumika katika kufikia lengo la makala haya. Msingi wa Sanaa na jamii/fasihi na jamii ulitumika katika uchambuzi na uwasilishaji wa data za makala haya.

Msingi wa fasihi na jamii ulitumika kuchambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika riwaya ya Kufikirika. Msingi huu mmoja uliotumika katika makala haya ni faafu katika kukamilisha lengo la utafiti huu.

3. MBINU YA UTAFITI

Ponera (2019), ameeleza kuwa, mbinu ya utafiti ni vipengele muhimu vinavyotakiwa kuzingatiwa katika lengo la utafiti. Sehemu ya kujibu maswali kama vile, nini kifanyike, lini, nani na namna gani. Data zauwandani kutoka mkoa wa Kilimanjaro, wilaya ya Same vijijini, mahususi katika kijiji cha Vuje, kitongoji cha Mgambo na data kutoka maktabani zilitumika kuandaa makala haya. Data hizo zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya udodosaji na mbinu ya usomaji maktabani. Mbinu ya udodosajiilihusisha watafitiwa kumi (10) katika kujibu maswali kwa kujaza majibu yaliyohusiana na mada ya utafiti. Mtafiti alitumia mbinu ya usomaji maktabani kwa kusoma kitabu kimoja cha riwaya ya Kufikirika. Katika utafiti wa makala haya mtafiti alitumia sampuli ya watafitiwa 10. Miongoni mwa watafitiwa hao kulikuwa na watu wazima kuanzia miaka 40 na kuendelea ambao ni wazawa na wenyeji wa kabila la Wapare na vijana kuanzia miaka 20 hadi 35 ambao ni Wapare.

Sampuli Lengwa tajwa mpokezano ilitumika katika utafiti wa makala haya. Huu ni usampulishaji ambao baada ya mtafiti kupata data kutoka kwa mtafitiwa mmoja uwandani mtafitiwa huyo alitumika kuelekeza sehemu ambayo anapatikana mtafitiwa mwingine wa kupata data za utafiti huu.(Abdallah, 2021). Sampuli hii ilihusisha watafitiwa kumi katika kujibu maswali kwa kujaza majibu yaliyohusian na mada ya utafiti. Yaani, tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika riwaya ya Kufikirika. Watafitiwa walielezea tija mbalimbali zilizodhihirisha mwangwi wa falsafa ya Wapare.

Pia katika mbinu ya usomaji maktabani, mtafiti alichambua tija mbalimbali zilizodhihirisha mwangwiwa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika. Mbinu zote mbili, yaani mbinu ya udodosaji na mbinu ya usomaji maktabani, zilitumika katika kukamilisha lengo la utafiti wa makala haya. Lngo hilo ni kuchambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika riwaya ya Kufikirika.

Tija za Mwangwi wa Falsafa ya Wapare zinazodhihirika katika Riwaya ya Kufikirika

Wapare wa wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo wana falsafa yao ambayo ina tija zake ambazo ni mwangwi katika riwaya ya Kufikirika. Kuna baadhi ya falsafa ambazo kwa mujibu wa taarifa za watafitiwa, zimeonekana kuwa na tija katika jamii. Watafitiwa waliotumika ni watu wa umri wa utu uzima kuanzia miaka 40 na kuendelea ambao ni wenyeji na wazawa wa jamii ya Wapare. Data zilizokusanywa zilihusiana na tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika. Ukusanyaji wa data ulitumia njia ya dodoso na njia ya usomaji maktabani. Baadhi ya mila zinazotekelezwa katika jamii ya Wapare zina faida kwa jamii husika. Kwa mujibu wa taarifa za watafitiwa uwandani imeonekana kuwa, zipo baadhi ya mila zinazoendelea kutendeka katika jamii ya Wapare ambazo zinafaa kuenziwa kutokana na tija/faida zake. Tija za falsafa ya Wapare zimeonekana kuwa na mwangwi katika riwaya ya Kufikirika kama ifuatavyo:

Husaidia kuponesha maradhi mbalimbali

Suala la kuponesha maradhi mbalimbali limeelezewa katika jamii ya Wapare kwa namna yake. Suala hili limewekewa msisitizo katika mhimili wa Sanaa na jamii kupitia Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili wa sana na jamii ni kwamba, mambo yaliyoelezwa katika kazi za fasihi yana lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii kuhusiana na suala la kuponesha maradhi.

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (263-273), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Fasihi kama kazi ya kisanaa, haiwezi kujitenga na jamii kwa kuwa, masuala yaliyoelezwa katika kazi za fasihi, yanasadifu yaliyomondani ya jamii husika. Suala hili limedhihirika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii jamii inayopatikana katika jamii ya Wapare wa wilaya ya Same vijijiji, mahususi katika kijiji cha Vuje kitongoji cha Mgambo. Suala hili limeelezwa na mtafitiwa na.1 kupitia njia ya udodosaji akieleza kuwa:

Data ya 1: Njia ya Udodosaji

Yapo maradhi yanayoshindikana kutibika hospitalini na kulazimika kutumia dawa za asili na hatimaye mgonjwa kupona. Pia mtu huweza kupona maradhi na matatizo mbalimbali baada ya kufanyiwa tambiko. Yawezekana mtu anaumwa mara kwa mara kwa sababu ya madai fulani ya mizimu ya kwao, akishatekeleza kutoa madai yanayotakiwa hupata ahueni.

(Chanzo: Njia ya UdodosajiUtafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa, kuna faida za kutekeleza masuala mbalimbali ya mila kwasababu, kuna manufaa makubwa katika kutibia baadhi ya maradhi ambayo yameshindikana kutibika kwa kutumia dawa za hospitalini. Katika riwaya ya Kufikirika, suala hili limeoneshwa na waganga ambao walimtibia Mfalme na Malkia ambao walikuwa na tatizo la kutopata mtoto kwa muda mrefu. Mfalme na Malkia walipatiwa tiba za asili na hatimaye kufanikiwa kupata mtoto. Mwandishi amelithibitisha hili akieleza:

Data ya 1:Usomaji Maktabani

Uzito na vyeo vya hirizi vilikuwa mbalimbali, palikuwa na hirizi ndogo za uzito wa wakia moja na kubwa za uzito na wakia mbili, hata ratili moja. Wagonjwa walipewa kuvaa hirizi hizi na ilisemwa kuwa zilipovaliwa na mgonjwa nafuu ilifuata mara moja (uk 10). Mfalme na Malkia walilemewa na uzito wa hirizi juu ya miili yao……walipoamriwa kuzivua……siku hiyo kuni, makaa na mafuta yote yalikwisha kwa kuchoma hirizi hizo. Moshi mwingi uliruka juu ukatanda katika hewa kama wingu kubwala mvua.(uk 11).

(Chanzo: Usomaji Maktabani Robert, 1967,uk 10-11).

Hapa ina maana kuwa, waganga wa hirizi walitumia hirizi hizo katika kumtibia Malkia na Mfalme ambao walisumbuliwa na tatizo la kutopata mtoto kwa miaka mingi. Hirizi hizo zilipovaliwa zilisaidia kwa kumpa mgonjwa nafuu. Baada ya hirizi hizo kutumika, ziliteketezwa kwa moto. Mwandishi anaendelea kuelezea mafanikio aliyoyapata Malkia kutokana na tiba za uganga akieleza kuwa:

“Baada ya mdua mdogo, neema ya Kufikirika ilianza kurudi, shida ikakimbia. Katika wakati huohuo habari ilinong’onwa na watumishi wachache katika nyumba ya Mfalme kuwa malkia alikuwa ana mimba…. Mwaka haukumalizika akazaliwa mtoto wa kiume. Mfalme na Malkia walifurahi mno.

Mbele ya umati mkubwa kabisa wa watu Mfalme alihutubia Nimefurahi sana kwa kujaliwa kupata mtoto na nimependezwa mno na kazi zote zilizofanywa na kila kundi la waganga wangu. Kundi la watabiri limefaulu na kuwa limeshinda makundi mengine yote. Kila mganga katika kundi hili atapewa ijara mara mbili” shangwe!

(Chanzo: Usomaji Maktabani Robert, 1967, uk 17-18).

Hapa mwandishi ana maanisha kuwa, suala la uganga na tiba za dawa za asili zimeleta mafanikio chanya yaliyotarajiwa na jamii husika, kwani matatizo yaliyowasibu wanajamii yalitatulika kupitia uganga wa dawa za asili. Sehemu hii imethibitisha kuwepo kwa Mwangwi wa falsafa ya Wapare kwani yaliyoandikwa na mtunzi wa riwaya teule ya Kufikirika yamesadifu falsafa ya uganga iliyopo katika jamii ya Wapare ambayo inautazama uganga ikiwa ni falsafa muhimu sana katika ustawi wa maisha ya jamii zao. Suala la uganga ni falsafa muhimu sana inayotekelezwa na jamii ya Wapare.Uganga umepewa uzito kutokana na umuhimu wake kwa jamii ya Wapare na katika riwaya ya Kufikirika kama ilivyoelezwa hapo juu. Kwa hiyo, taarifa hizo mbili,yaani kutoka uwandani na kutoka maktabani, zinaonesha mshabaha uliopo baina ya Wapare na maelezo ya mhimili kama ulivyokwisha tajwa hapo awali, kwani huenda sambamba na hoja husika.

Husaidia katika ulinzi wa jadi

Masuala ya mila husaidia katika ulinzi wa jadi na hivyo kupunguza mambo mbalimbali ya uhalifu. Masuala ya mila yanafanywa na wazee wa kimila pamoja na waganga wa jadi. Maisha ya jamii ya Wapare yametawaliwa na shughuli za jadi na matumizi ya dawa za kienyeji. Suala hili limeelezwa katika jamii hii kwa upana wake. Jambo hili limesisitizwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa

katika kazi za fasihi, yanakuwa na lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii husika unaohusu ulinzi wa jadi. Suala hili limesadikika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wa wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo, kupitia watafiti mbalimbali kwa kutumia njia ya udodosaji mt 2 akieleza kuwa:

Data ya 2: Njia ya Udodosaji

Mila husaidia katika ulinzi wa jadi na hivyo kupunguza uhalifu mfano zipo dawa za kukamata wezi na wachawi, dawa hizi huwekwa shambani kwajili ya kuwafanya wezi wagande shambani pindi wanapoiba mazao. Pia huweza kuwagandisha wachawi wanapokuja kuwanga katika nyumba usiku, unaweza kumkamata mchawi nje kwako asubuhi akiwa anaambaa ambaa uwanjani au nje ya nyumba yako.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa, matumizi ya baadhi ya dawa za asili husaidia katika kuimarisha ulinzi wa familia na kwani unawafanya wahalifu wanase pindi wanapofanya uhalifu wao na hatimaye wanajamii kuwakuta wameganda hadharani. Hali hii huwafanya wahalifu waone aibu na kwao kuwa ni fedheha kubwa, hivyo wengine kutothubutu kufanya uhalifu kwaajili ya kulinda heshima ya familia zao na jamii kwa ujumla. Falsafa ya ulinzi wa jadi inadhihirika katika riwaya ya *Kufikirika* pale ambapo mwandishi anaeleza matumizi ya hirizi zilizotumika kuzuia matatizo mbalimbali mwandishi amelithibitisha hili akieleza:

Data ya 2: Njia ya Usomaji Maktabani.

Uzito na vyeo vya hirizi vilikuwa mbalimbali, palikuwa na hirizi ndogo za uzito wa wakia moja na kubwa za uzito na wakia mbili, hata ratili moja. Wagonjwa walipewa kuvaa hirizi hizi na ilisemwa kuwa zilipovaliwa na mgonjwa nafuu ilifuata mara moja (Uk10-11).

(Chanzo: Njia ya Usomaji Maktabani Robert, 1967 Uk 10-11).

Jambo hili limesisitizwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi, yanakuwa na lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii husika unaohusu ulinzi wa jadi. Hivyo, data za hapo juu, yaani uwandani na maktabani zimechambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika.

Hudumisha mila na desturi za jamii

Masuala ya matambiko na uganga hudumisha mila na desturi za jamii. Maisha ya jamii ya Wapare yametawaliwa na masuala ya matambiko na uganga. Suala hili limeelezewa katika jamii hii kwa upana wake. Suala hili linasadikika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wanaopatikana katika wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo, kupitia mtafitiwa na.3 kwa njia ya udodosaji akieleza kuwa:

Data ya 3: Njia ya Udodosaji

Matambiko na uganga hudumisha mila na desturi za jamii ya Wapare toka kizazi hadi kizazi kingine, kwani kufanyika kwa mambo haya huwa ni muendelezo wa yale yaliyoachwa na vizazi vilivyopita.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa, masuala ya uganga na matambiko husaidia katika kudumisha mila na desturi za jamii husika kutokana na kuwa yapo masuala ya uganga na matambiko kwa jamii ya Wapare ambayo huendelea kutendeka kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine, na hivyo kufanya mambo hayo kuenziwa na kutosahaulika katika jamii husika. Pia suala hili linadhihirika katika riwaya ya *Kufikirika*pale ambapo mwandishi alipoonesha masuala ya matambiko na kafara katika kuponya maradhi mbalimbali mfano tatizo la Mfalme na malkia la kutopata mtoto kwa muda mrefu. Jambo hili limesisitizwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi, yana lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa unaohusu kudumisha mila na desturi za jamii.

Data ya 3: Njia ya Usomaji Maktabani

Kundi la waganga wa kafara ni kundi la watu ambao walijipambanua kwa kuponya aina kadhaa wa kadhaa za maradhi kwa makafara ya vitu vidogo vidogo kama vile mayai, njiwa au kuku….Wafikirika walisadiki sana kuwa, makafara ya waganga hao yaliweza kufukuza baa au maradhi .

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (263-273), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

(Chanzo: Usomaji Maktabani 2025 Robert, 1967,uk 9).

Hapa inaonesha kuwa katika matambiko kuna utoaji wa sadaka ya vitu mbali mbali kama vile mayai, njiwa au kuku na vitu vingine. Suala hili liliaminika katika kusaidia kukamilisha suala zima la kuondoa matatizo yanayosumbua watu. Hivyo, data zote mbili, yaani, kutoka uwandani na maktabani zimechambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika.

Husaidia kuleta mvua

Masuala ya matambiko husaidia katika kuleta mvua. Maisha ya jamii ya Wapare, yametawaliwa na masuala ya matambiko. Suala hili limeelezewa katika jamii hii kwa namna yake. Jambo hili limesisitizwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi,yana lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii lengwa.

Suala hili linathibitika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wanaopatikana katika wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo kupitia tafitiwa na.4 kwa njia ya udodosaji akieleza kuwa:

Data ya 4: Njia ya Udodosaji

Matambiko husaidia katika kuleta mvua, mfano matambiko ya ukoo wa Wajema ni maarufu sana katika kuifanya mvua inyeshe baada ya ukame au jua la muda mrefu. Pia upo msitu wa Wagonja unaojulikana kama msitu wa Kolongia, msitu huu upo katika kitongoji cha Mgambo, hutumika katika matambiko ya mvua. Mara nyingi matambiko ya kuleta mvua hutumia zaidi wanyama kama vile kondoo dume mweusi au ng'ombe dume mweusi asiyekuwa na rangi mchanganyiko,pamoja na dawa mbalimbali za asili. Pia hutumia punje mbalimbali za nafaka kama vile mtama, mahindi, maharage, kunde, njugu, ufuta pamoja na mazao mengine kama viazi vitamu, mihogo na ndizi ng'ombe.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa,suala la tambiko la mvua kwa jamii ya Wapare, limepewa uzito wa namna yake, kwani imeelezwa kuwepo na utoaji wa wanyama maalumu kama vile kondoo ,ngo'mbe, nafaka kama vile punje za mtama, mahindi, maharage, kunde, njugu, ufuta pamoja na mazao mengine kama viazi vitamu, mihogo na ndizi ng'ombe. Vile vile matambiko ya mvua hufanyika katika mazingira maalumu yaliyoandaliwa kwa ajili ya shughuli hiyo kama vile katika msitu, mfano matambiko ya mvua ambayo hufanyika katika msitu wa Kolongia. Tambiko hili hufanyika hasa inapotokea ukame kwa muda mrefu kiasi cha kuathiri shughuli za kilimo na malisho ya wanyama. Kutokana na imani kali iliyopo miongoni mwa wanajamii, baada ya shughuli za tambiko kufanyika, mvua kubwa hunyesha na hatimaye watu kuendelea na shughuli za kilimo na kupata mazao mengi pamoja na malisho ya mifugo. Pia mwandishi ameionesha falsafa hii katika riwaya ya *Kufikirika* pale alipoeleza kuhusu matambiko yalivyosaidia kuleta mvua katika nchi ya Kufikirika na kuleta neema ya mazao.

Jambo hili limesisitizwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi,yana lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii lengwa. Mwandishi amelithibitisha hili akieleza kuwa:

Data ya 4: Njia ya Usomaji Maktabani

Serikali ya Kufikirika ililazimisha sana ustadi wa watu wake katika kazi zote, mbegu mbalimbali ziliagizwa kutoka nchi nyingine zikipandwa katika mashamba....."Baada ya mduo mdogo, neema ya Kufikirika ilianza kurudi, shida ikakimbia.

(Chanzo: Usomaji Maktabani Utafiti 2025, Robert,1967, uk 17-18).

Hapa ina maana kuwa, shughuli mbalimbali zilifanywa na wananchi wa Kufikirika kwa lengo la kuleta ustawi wa nchi yao. Hivyo, serikali ilijitahidi kuweka utaratibu wa kuwalazimisha wananchi wajishughulishe na fani mbalimbali ili kuinua uchumi wa nchi yao. Suala la uganga na tiba za dawa za asili zimeleta mafanikio chanya yaliyotarajiwa na jamii husika, kwani matatizo yaliyowasibu wanajamii yalitatulika kupitia uganga wa dawa za asili. Sehemu hii imethibitisha kuwepo kwa Mwangwi wa falsafa ya Wapare kwani yaliyoandikwa na mtunzi wa riwaya teule ya Kufikirika yamesadifu falsafa ya uganga iliyopo katika jamii ya Wapare ambayo inautazama uganga ikiwa ni falsafa muhimu sana katika ustawi wa maisha ya jamii zao.

Suala la uganga ni falsafa muhimu sana inayotekelezwa na jamii ya Wapare. Suala hili limedhihirika pia katika riwaya teule ya Kufikirika kama ambavyo imeelezewa hapo awali. Kwa hiyo, taarifa hizo mbili,yaani kutoka uwandani na kutoka katika kitabu, zinaonesha mshabaha uliopo baina ya Wapare na maelezo ya mhimili kama ulivyokwisha tajwa hapo awali, kwani huenda sambamba na hoja husika.

Husaidia kuendeleza maadili mema katika jamii

Maisha ya jamii ya Wapare yametawaliwa na masuala ya uganga na matambiko. Suala hili limeelezwa katika jamii hii kwa upana wake. Suala hili limeelezwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na Jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi, yana lengo la kufikisha ujumbe katika jamii iliyokusudiwa.Suala hili linathibitika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wanaopatikana katika wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo, kupitia mtafitiwa na 5 njia ya Udodosaji akieleza kuwa:

Data ya 5: Njia ya Udodosaji

Uganga na matambiko husaidia katika kuendeleza maadili mema katika jamii. Kuna suala la viapo, watu wanaoshiriki mila hizi hupewa miiko ya kutofanya mambo mabaya yaani kutowatendea mambo mabaya watu wengine. Katika kitongoji cha Mgambo kuna msitu wa matambiko unaojulikana kwa jina la msitu wa Mma, yaani msitu wa viapo ambao ukoo wa Wangulwi huutumia sana. Iwapo mtu ameshiriki katika masuala ya matambiko, kisha akatendea watu wengine mambo mabaya, anadhurika na hata kupoteza maisha iwapo hakuwahiwa kuopolewa (kuaguliwa) na wazee wa mila.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa, masuala ya uganga na matambiko, kwa jamii ya Wapare yameoewa uzito sana. Kutokana na imani kali iliyopo kwa wanajamii, mtu anayeshiriki masuala ya matambiko na uganga, hapaswi kabisa kuwatendea ubaya watu wengine, kwani huweza kupatwa na madhara makubwa sana kiasi cha kuweza kupoteza maisha iwapo hatopatiwa msaada wa matibabu (kuopolewa) kwa haraka. Suala hili linasaidia katika kupunguza uwezekano wa watu kufanyiana ubaya, kwani tayari watu huwa na hofu ya kudhurika iwapo watathubutu kutenda kinyume na miiko ya matambiko na uganga. Hali hii huwasaidia wanajamii kuishi kwa amani na upendo kwa kutenda yanayofaa katika jamii.

Falsafa hii inadhihirika katika riwaya ya *Kufikirika* pale ambapo jamii imeonekana ikitekeleza masuala ya matambiko katika kuondoa mikosi na mabalaa ili jamii iishi kwa amani. Mwandishi amelithibitisha hili akieleza kuwa:

Data ya 5: Njia ya Usomaji Maktabani

Kundi la waganga wa kafara ni kundi la watu ambao walijipambanua kwa kuponya aina kadhaa wa kadhaa za maradhi kwa makafara ya vitu vidogo vidogo kama vile mayai, njiwa au kuku….Wafikirika walisadiki sana kuwa, makafara ya waganga hao yaliweza kufukuza baa au maradhi ....“Baada ya mduomdogo, neema ya Kufikirika ilianza kurudi, shida ikakimbia.

(Chanzo: Usomaji Maktabani 2025 Robert, 1967,uk 9-17).

Hapa inaonesha kuwa katika matambiko kuna utoaji wa sadaka ya vitu mbali mbali kama vile mayai, njiwa au kuku na vitu vingine. Suala hili liliaminika katika kusaidia kukamilisha suala zima la kuondoa matatizo yanayosumbua watu. Hivyo, data za hapo juu,yaani uwandani na maktabani zimechambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika.

Husaidia kustawisha mazao.

Maisha ya jamii ya Wapare, yametawaliwa na masuala ya matumizi ya dawa za asili katika mazao tangu yanapokuwa shambani. Suala hili limeelezwa katika jamii hii kwa namna yake. Suala hili limeelezwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi, yana lengo ka kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa kuhusiana na kustawisha mazao. Suala hili linadhihirika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wanaopatikana katika wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo kupitia mtafitiwa na.6 kwa njia ya usaili akieleza kuwa:

Data ya 6: Njia ya Udodosaji

Wapare wengi wanatumia dawa za kinga za shambani zinazojulikana kwa jina la *Ihande*. Dawa hizi zinaposambazwa shambani, mazao yaliyomo humo hayapatwi na dhoruba yoyote ya magonjwa ya mimea. Pia kuna baadhi ya watu wenye tabia za *kung'wasa* mazao shambani (kupiga zongo au kuharibu mazao kichawi), shamba linapo sambazwa dawa hizi, dhoruba zote hizi hupitia mbali kabisa.

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (263-273), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa, Wapare wana dawa za asili ambazo wanazitumia shamani katika kukinga mazao yao yasiharibiwe na watu wenye macho mabaya (husda) ya kichawi. Dawa hiyo hutumika katika kusambaziwa mazao shambani, na hivyo huwa na matokeo mazuri, kwani mazao hustawi vizuri na kupata mavuno ya kutosha. Suala hili limedhihirika katika riwaya ya Kufikirika pale ambapo baada ya utekelezaji wa makafara na matambiko na hatimaye neema ya Kufikirika ilionekana. Mwandishi amelithibitisha hili akieleza kuwa:

Data ya 6:Njia ya Usomaji Maktabani

Wafikirika walisadiki sana kuwa, makafara ya waganga hao yaliweza kufukuza baa au maradhi ...."Baada ya mduo mdogo, neema ya Kufikirika ilianza kurudi, shida ikakimbia.

(Chanzo: Usomaji Maktabani 2025 Robert, 1967,uk 9-17).

Hapa ina maana kuwa, matumizi ya makafara yalisaidia kuondoa maradhi na shida mbalimbali zilitoweka na hatimaye neema ya nchi ya Kufikirika kuonekana. Hivyo,data za hapo juu yaani uwandani na maktabani, zimechambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika.

Husaidia wanajamii kuishi kwa kuaminiana.

Jamii ya Wapare walio wengi, huishi maisha yao katika hali ya kuaminiana. Suala hili limeelezewa katika jamii hii kwa namna yake. Suala hili limeelezewa katika mhimili wa tano wa Sanaa na Jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi, yana lengo la kufikisha ujumbe katika jamii iliyokusudiwa la kufanya wanajamii kuishi kwa kuaminiana. Suala hili linathibitika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wa wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo, kupitia mtafitiwa 7 kwa njia ya Udodosajiwakieleza kuwa:

Data ya 7: Njia ya Udodosaji

Jamii ya Wapare walio wengi, wamekuwa wakiishi kwa kuaminiana. Wanajamii wamekuwa wakila yamini, mfano: kupitia viapo mbalimbali

(*mma),* wanajamii walioshiriki masuala haya walikula yamini ya kutofanyiana ubaya katika familia zao.

Watu waliokula kiapo hiki iwapo mmojawapo atafanya kinyume na miiko waliyojiwekea, anaweza kupata madhara makubwa sana, kiasi cha kuweza kupoteza maisha iwapo hatopatiwa msaada wa matibabu kutoka kwa wazee wa mila.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa, kutokana na imani kali iliyopo kwa wanajamii, mtu anayeshiriki masuala ya viapo hapaswi kabisa kuwatendea ubaya watu wengine, kwani huweza kupatwa na madhara makubwa sana kiasi cha kuweza kupoteza maisha iwapo hatopatiwa msaada wa matibabu kutoka kwa wazee wa mila. Jambo hili hula kama zuio la kuwafanya watu wasitendeane mambo mabaya, hivyo, husaidia watu kuishi kwa amani na upendo kwani huaminiana miongoni mwao. Katika riwaya ya *Kufikirika* suala hili linadhihirika pale ambapo waganga waliaminiwa na kushikirikiana katika kumtibu mke wa mfalme na kupata mtoto.Kwa kulithibitisha hili mwandishi ameeleza:

Data ya 7: Njia ya Usomaji Maktabani

"Baada ya mdua mdogo, neema ya Kufikirika ilianza kurudi, shida ikakimbia. Katika wakati huo huo habari ilinong'onwa na watumishi wachache katika nyumba ya Mfalme kuwa malkia alikuwa ana mimba…. Mwaka haukumalizika akazaliwa mtoto wa kiume. Mfalme na Malkia walifurahi mno.

(Chanzo: Usomaji Maktabani Robert, 1967, uk 17-18).

Hapa ina maana kuwa, waganga wa Kufikirika waliaminiwa katika kutibu tatizo la mfalme na malkia la kutopata mtoto kwa muda mrefu. Kwa kufanya hivyo, waliwatibia mfalme na malkia na hatimaye kufanikiwa kupata mtoto. Data zote yaani, kutoka uwandani na maktabani, zimeonesha uwepo wa tija za mwangwi wa fasafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika kama zilivyochabuliwa hapo ju

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (263-273), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Huisaidia jamii katika kudumisha umoja na mshikamano.

Maisha ya jamii ya Wapare walio wengi, huishi maisha yao katika hali ya kushirikiana katika mambo mbalimbali. Suala hili limeelezwa katika jamii hii kwa nana yake. Suala hili limeelezewa katika mhimili wa tano wa Sanaa na Jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi yana lengo la kufikisha ujumbe katika jamii iliyokusudiwa wa kudumisha umoja na mshikamano. Suala hili linathibitika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wanaopatikana katika wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo, kupitia mtafitiwa na.8 kwa njia ya udodosaji ameeleza kuwa:

Data ya 8: Njia ya Udodosaji

Jamii ya Wapare walio wengi, hufanya shughuli zao mbalimbali kwa kushirikiana. Mfano kupitia shughuli kama vile sherehe, ugonjwa, majanga na misiba, watu hushirikiana na hivyo kudumisha umoja katika jamii.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa inamaana kuwa, wanajamii hushirikiana kwa kukimbiliana katika masuala ya kijamii ya shida na raha. Mfano hushirikiana pamoja katika sherehe mbalimbali, misiba, ugonjwa na majanga mbalimbali. Sulla hili hudumisha umoja na mshikamano katika jamii. Kwa upande wa riwaya ya Kufikirika, suala la ushirikiano limeelezewa namna ambavyo Wafikirika walikuwa na umoja katika kutekeleza mambo yao. Kwa kulithibitisha hili mwandishi ameeleza kuwa:

Data ya 8 : Njia ya Usomaji Maktabani

Wafikirika walikuwa na umoja madhubuti ambao walisimama imara mbele ya machafuko yoyote, shauri moja jema lilikubaliwa na kushangiliwa na wote na baya lilikataliwa na kila mtu. (Uk 15).

Hapa ina maana kuwa, wananchi wa Kufikirika walikuwa na umoja imara,walishirikiana katika kutenda mema na hata kuwa na umoja katika kukataa yasiyofaa. Data zote yaani, uwandani na maktabani zinaonesha tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika kama ambavyo imeelezewa hapo juu.

Huleta ustawi wa familia.

Masuala mbalimbali ya kijamii kama ndoa na uzazi husaidia katika ustawi wa jamii. Jamii ya Wapare walio wengi hudumisha masuala yao ya uzazi na ndoa ambayo huwasaidia katika kujenga ustawi wa jamii zao. Suala hili limeelezwa katika jamii hii kwa upana wake. Suala hili limeelezwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na Jamii katika Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi yana lengo la kufikisha ujumbe katika jamii iliyokusudiwa kuhusu kuleta ustawi wa familia.

Suala hili linathibitika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wa Wilaya ya Same vijijini mahususi kijiji cha Vuje katika kitongoji cha Mgambo kupitia mtafitiwa na.9 kwa njia ya udodosaji akieleza kuwa:

Data ya 9: Njia ya Udodosaji

Jamii ya Wapare hudumisha masuala ya ndoa na uzazi, hii husaidia katika kujenga familia, kwani familia ni watoto, na watoto ndio taifa la kesho ambalo hujengwa na wazazi wa sasa. Hivyo, kuwa na familia ni jambo jema sana katika jamii.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa,suala la uzazi na ndoa katika jamii, husaidia katika kuleta ustawi katika jamii husika,hivyo,ni suala ambalo limepewa kipaumbele sana katika jamii ya Wapare kutokana na umuhimu wake kwa jamii hiyo, kwani ndio chanzo cha kuwepo kwa familia. Katika riwaya ya *Kufikirika* jambo hili linadhihirika pale ambapo waganga walifanya juhudi za kumtibu mke wa mfalme hadi kupata mtoto.Mwandishi amelithibitisha hili akieleza kuwa:

Data ya 9: Njia ya Usomaji Maktabani

Wafikirika walisadiki sana kuwa, makafara ya waganga hao yaliweza kufukuza baa au maradhi ....Katika wakati huo huo habari ilinong'onwa na watumishi wachache katika nyumba ya Mfalme kuwa malkia alikuwa ana mimba…. Mwaka haukumalizika akazaliwa mtoto wa kiume. Mfalme na Malkia walifurahi mno.

(Chanzo: Usomaji Maktabani Robert, 1967, uk 17-18).

Hapa imeoneha namna ambavyo watu wa Kufikirika wamethamini suala la kuwa na familia. Suala hili lilionekana kuwa na uzito baada ya waganga na wananchi wa Kufikirika walivyofanya juhudi katika kuhakikisha kuwa, tatizo la mfalme na malkia la kutopata mtoto kwa muda mrefu linapatiwa tiba na hatimaye kufanikiwa kupata mtoto.Kwa hiyo, data za hapo juu yaani data za uwandani na maktabani zimeonesha uwepo wa tija za falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika.

Husaidia kuongeza ukoo.

Jamiiya Wapare walio wengi, wamekuwa na utaratibu wa kuwa na watoto wengi. Suala hili limeelezwa katika jamii hii kwa namna yake. Suala hili limeelezwa katika mhimili wa tano wa Sanaa na Jamii kupitia Nadharia ya Elimu Jamii. Katika mhimili huu ni kwamba, yaliyoelezwa katika kazi za fasihi, yanakuwa na lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii husika katika suala zima la kuongeza ukoo. Suala hili linadhihirika kupitia hali halisi inayopatikana katika jamii ya Wapare wa wilaya ya Same vijijini katika kitongoji cha Mgambo kupitia mhusika na.10 kwa njia ya udodosaji akieleza kuwa:

Data ya 10: Njia ya Udodosaji

Kwa jamii ya Wapare kumekuwa na suala la kuongeza ukoo kupitia falsafa ya familia pana. Kupitia falsafa hii, ukoo huwa mkubwa, kwani mtu mmoja (mume) kuwa na wanawake wengi, husaidi pia kuwa na watoto wengi watakao ongeza ukoo ambao ndio taifa lijalo.

(Chanzo: Njia ya Udodosaji Utafiti, 2025).

Hapa ina maana kuwa, baadhi ya falsafa za jamii ya Wapare, zimeonekana kuwa na manufaa mbalimbali katika jamii, hivyo, zinafaa kuenziwa na wanajamii. Pamoja na kuwa baadhi ya falsafa zimeonekana kuwa na manufaa kwa jamii kama walivyoelezea watafiti, kuna baadhi ya mila kama vile uzazi na ndoa , huendelezwa au kufanywa na baadhi ya ukoo au familia. Jamii ya Wapare inaendelea kuipa kipaumbele sana, kwani kila mwanajamii huona fahari kuwa na familia yake ambayo ndiyo itakayoendeleza mali zitakazoachwa na wazazi baada ya kutoweka duniani. Hivyo, watu huthamini sana kuwa na watoto wao wa damu na si kuazima kutoka kwa watu wengine. Tija ya mwangwi wa falsafa ya Wapare imepatikana kupitia falsafa ya familia pana ambayo husisitiza zaidi kuwa na familia kubwa.

Vijana wengi kuanzia miaka thelathini wana watoto sita hadi saba na kuendelea ingawa vijana hawaoi wake wengi wakaishi nao kwa pamoja kama ilivyo kuwa kwa wazee wa Kipare wa zamani. Lakini kwa vijana wanaweza kuwa na watoto wengi kupitia wake tofauti tofauti, na vijana huwa na sera ya kuongeza ukoo. Suala hili pia limeelezwa katika riwaya teule ya *Kufikirika*, ambapo mwandishi Shaaban Robert ameeleza namna ambavyo wananchi wa Kusadikika wamekuwa na utamaduni wa kuzaa watoto wengi ambao ndio huongeza nguvu kazi ya taifa. Kwa njia ya usomaji maktabani mwandishi amethibitisha hili katika sehemu ya utangulizi kwa kusema:

Data ya 10: Njia ya Usomaji Maktabani

Wafikirika ni wengi, nao ni wazazi mno. Nyumba moja kuwa ina watoto wanane hata kumi na sita si jambo la ajabu. Jumla ya wafikirika karibu sawa na nusu moja ya watu wa makabila yote mengine yaliyomo duniani….

(Chanzo: Usomaji Maktabani 2025 Robert,1967uk vii).

Hapa ina maana kuwa, suala la kuzaa watoto wengi kwa wananchi wa Kufikirika, ni suala ambalo limepewa kipaumbele sana, kwani kila nyumba ilionekana kuwa na watoto wengi, yaani kuanzia watoto sita na kuendelea. Suala la kuzaliana kwao ni jambo la fahari kwani limepewa uzito mkubwa na jamii. Kwa hiyo, taarifa hizo mbili, yaani kutoka uwandani na kutoka katika kitabu, zinaonesha mshabaha uliopo baina ya jamii ya Wapare na maelezo ya mhimili kama ulivyokwisha tajwa hapo awali.

4. HITIMISHO

Makala haya yamechambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirikakwa kuelezea tija hizo. Makala haya ni muhimu kwa wadau wote wa elimu na jamii kwa ujumla. Mahususi kwa wadau wa kazi za kifasihi, kwani fasihi haitenganishwi na jamii kwa kuwa, fasihi huwa na lengo la kufikisha ujumbe kwa jamii kutokana na yaliyomo ndani ya jamii husika.

Hivyo, kuna umuhimu wa kuwepo kwa makala yatakayochambua tija za mwangwi wa falsafa ya Wapare katika riwaya ya Kufikirika. Vile vile, makala haya ni faafu kwa marejeleo ya tafiti zijazo, mahususi tafiti za uga wa fasihi kwa ujumla. Zaidi ya hapo, makala haya ni hazina ya utamaduni wa jamii za kitanzania na Afrika kwa ujumla wake, kwa kutunza kumbukumbu kwa faida ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

MAREJELEO

[1] Abdallah, H.K. (2021).*Ujumi katika malumbano ya watani: Mifano ya familia za Wadigo wa Tanga mjini.* Chuo Kikuu cha Dodoma.

[2] Chuachua, R. (2016*). Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euprase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu*. Chuo Kikuu Cha Dodoma.

[3] Cooper, J.M. (Mh.). (1997). *Plato: Complete works.* Hackett Publishing Company.

[4] Johnston, D. (2006). *A Brief History of Philosophy.* Oxford University Press.

[5] Madumula, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi.*Sitima Printers and Stationers.

[6] Menand, L. (Mh.).(199). *Pragmatism: A reader*. Vintage Books.

[7] Nails, D. (2002). *The people of Plato: A prosopography of Plato and other Socratics*. Hachette.

[8] Nyiremba, S. D & Ishumi, A.G. M. (2002, 2003, 2004). *Phylosophy of Education: An Introduction to Concept.* Dar es Salaam University Press.

[9] Ponera, A. (2010). *Ufutuhi katika nathari za Shaaban Robert: Maana zake, sababu za kutumiwa na athari zake kwa jamii.* Chuo Kikuu cha Dodoma.

[10] Ponera, A. (2019). *Misingi ya Utafiti na Uandishi wa Kazi zaKitaamuli.* Cenral Tanganyika Press.

[11] Robert, S. (1967).*Kufikirika.* Oxford University Press.

[12] Senkoro, F. E. M. K (1982). Fasihi na Jamii. Press and Publicity Centre..

[13] Taine, H.(1864). *History of English Literature*. Hachette.

[14] TUKI (2002). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.

[15] TUKI (2004). *Kamusi ya KiswahiliSanifu.* Oxford University Press.